Arusha, Tanzania

Tovuti: [www.african-court.org](http://www.african-court.org)

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

MUHTASARI WA HUKUMU

**SONG LEI**

**DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OMBI NAMBA 066/2019**

**JUDGMENT ON MERITS AND REPARATIONS**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Mjini Arusha, tarehe 6 Machi 2026**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) ilitoa hukumu katika kesi ya *Song Lei dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Song Lei (Mlalamikaji) ni mfanyabiashara na raia wa Jamhuri ya Watu wa China anayeishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Taifa Lililoshtakiwa). Wakati wa kuwasilisha Ombi hili, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Ukonga, Dar es Salaam, baada ya kesi yake kusikilizwa, kupatikana na hatia, na kuhukumiwa kifungo cha miaka 20 jela kwa, miongoni mwa mambo mengine, biashara haramu ya nyara na kumiliki nyara za serikali kinyume cha sheria, hususan pembe za kifaru. Anadai kwamba kulikuwepo ukiukwaji wa haki zake wakati wa kesi katika mahakama za Tanzania.

Taifa Lililoshtakiwa lilipinga mamlaka ya Mahakama kusikiliza shauri hilo pamoja na ukubalifu wa Ombi hilo.

Kuhusu mamlaka ya Makahama, Taifa Lililoshtakiwa lilizua pingamizi dhidi ya mamlaka ya Mahakama kusikiliza kesi zenye madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Hasa, Taifa Lililoshtakiwa lilidai kuwa Mahakama hii inatumiwa kutathmini Ushahidi na, kwa hivyo, kufanya kazi kama mhakama ya rufaa ilhali haina mamlaka hayo. Zaidi ya hayo, Taifa Lililoshtakiwa lilidai kuwa Mwombaji haoneshi uhusiano wowote kati ya uendeshaji mashtaka wenye makosa wa mahakama za ndani na madai ya ukiukaji wa haki za binadamu.

Kuhusu madai kuwa Mahakama itakuwa ikitekeleza mamlaka ya rufaa, Mahakama ilieleza tena falsafa yake ya sheria kwamba haitekelezi mamlaka ya rufaa kuhusiana na madai ambayo tayari yamechunguzwa na mahakama za kitaifa. Wakati huo huo, hata hivyo, na hata ingawa Mahakama si mahakama ya rufaa ikilinganishwa na mahakama za ndani, bado ina

mamlaka ya kutathmini uhalali wa kesi za ndani dhidi ya viwango vilivyowekwa katika hati za kimataifa za haki za binadamu zilizoidhinishwa na Taifa linalohusika. Katika kutekeleza shughuli iliyotajwa hapo juu, Mahakama iliamua, kwamba kwa namna hiyo haiwi mahakama ya rufaa.

Kuhusu pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa kwamba Mwombaji hakuonesha uhusiano wowote kati ya uendeshaji mashtaka wenye makosa wa mahakama zake za ndani na madai madai ya ukiukaji wa haki za binadamu, Mahakama iliamuwa kwamba hili ni suala litakaloshughulikiwa kwa kuzingatia ustahili wake na wala halihusiani na kuamuliwa kwa mamlaka yake.

Kuhusu pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa kwamba Mahakama hiyo haikuwa na mamlaka ya kufutilia mbali mashtaka yote yaliyokuwa yanaendelea na yaliyo katika mahakama za rufaa, Mahakama ilirejelea Ibara ya 27(1) ya Protokali, na kuhitimisha kuwa ina mamlaka ya kutoa aina mbalimbali za fidia, ikiwa ni pamoja na amri ya kubatilisha mashtaka yaliyo katika mahakama za kitaifa, amri ya kubatilisha upatikanaji wa hatia na hukumu, na kuamrisha kuachiliwa kwa Mwombaji kutoka gerezani, mradi tu ukiukaji unaodaiwa umethibitishwa.

Mahakama ilibainisha zaidi kwamba kwa kuzingatia kuwa madai ya ukiukaji yaliyowasilishwa mbele yake yanahusu haki zilizoelezwa katika Mkataba, ambao Taifa Lililoshtakiwa ni Mshirika, ilikuwa na mamlaka ya kisheria ya kuchunguza Ombi hilo.

Kwa sababu hizi, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi iliyotolewa na Taifa Lililoshtakiwa kuhusu mamlaka yake ya kuwa mwamuzi wa shauri hilo.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Taifa Lililoshtakiwa, hata hivyo Mahakama ilivichunguza. Kuhusiana na hilo, Mahakama iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya kutoa maamuzi kwa sababu, tarehe 29 Machi 2010, Taifa Lililoshtakiwa liliweka Azimio linalozungumziwa katika Ibara ya 34(6) ya Protokali, ambayo inaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Taifa Lililoshtakiwa kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) ya Protokali. Mahakama ilisisitiza kwamba hali ya Taifa Lililoshtakiwa kuondoa Azimio hilo, tarehe 21 Novemba 2019, haikuathiri Ombo hili kwa kuwa kujiondoa kulianza rasmi tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa baada ya Ombi hili kuwasilishwa, tarehe 17 Desemba 2019.

Mahakama pia iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Taifa Lililoshtakiwa kuwa mshirika wa Protokali hii. Mwisho, ilitambua kwamba ilikuwa na mamlaka ya kieneo kwa kuwa matukio yanayozungumziwa yalitokea katika eneo la Taifa Lililoshtakiwa, ambalo ni mshirika wa Mkataba na Protokali.

Mahakama ilisema kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 6(2) ya Protokali, lazima ifanye uamuzi kuhusu ukubalifu wa kesi zote zilizofikishwa mbele yake. Kuhusu Ombi hili la sasa, Taifa Lililoshtakiwa lilitoa pingamizi kuhusu ukubalifu wa Ombi kwa kurejelea kutotumia kikamilifu njia zote za usuluhishaji za ndani.

Kuhusu pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa kwamba Mwombaji alikosa kutumia njia zote za usuluhishaji za ndani, Mahakama iliamua kuwa Mwombaji alitumia kikamilifu njia zote za usuluhishaji za ndani kwa kuwa Mahakama ya Rufaa ya Taifa Lililoshtakiwa, chombo cha juu zaidi cha mahakama katika Taifa Lililoshtakiwa, lilikubaliana na kutiwa kwake hatiani na hukumu iliyotolewa, kufuatia kesi ambapo Taifa Lililoshtakiwa lilikuwa na nafasi ya kuzungumzia ukiukaji uliodaiwa na Mwombaji kuwa ulitokana na kesi na rufaa yake. Kwa sababu hii, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi za Taifa Lililoshtakiwa kuhusu ukubalifu wa Ombi hilo.

Mahakama ilisema kuwa hakuna pingamizi iliyotolewa kuhusu mahitaji mengine ya ukubalifu, hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni 50(1) ya Kanuni hizo, ilitathmini vigezo vyote vya vilivyoelezwa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni hizo, ambayo kimsingi inataja tena vifungu vya Ibara ya 56 ya Mkataba, ili kuhakikisha kwamba Ombi hilo lilitimiza viwango vinavyohitajika.

Kwa mantiki hiyo, Mahakama iliamua kwamba Mwombaji alikuwa ametambuliwa wazi kwa jina, na kutimiza Kanuni ya 50(2) ya Kanuni hizo. Pia iliamua kwamba madai ya Mwombaji yalikusudia kuzilinda haki zake kwa mujibu wa Ibara ya 3(h) ya malengo ya Sheria ya Katiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo basi Ombi hilo lilizingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni hizo.

Zaidi ya hayo, Mahakama iliamua kwamba lugha iliyotumiwa katika Ombi haikuwa ya kudhalilisha au yenye matusi kwa Taifa Lililoshtakiwa au taasisi zake, na hivyo kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni hizo. Pia Ombi hilo halikujikita katika habari zinazosambazwa

kupitia kwa vyombo vya habari pekee, lilijikita pia kwenye hati za mahakama kutoka kwa mahakama za ndani za Taifa Lililoshtakiwa, likitimiza Kauni ya 50(2)(d) ya Kanuni hizo. .

Kuhusu hitaji kwamba Ombi liwasilishwe katika muda mwafaka, Mahakama ilibaini kwamba uamuzi wa mwisho wa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ulitolewa tarehe 30 Agosti 2019 na Mwombaji akawasilisha Ombi lake mbele ya Mahakama hii tarehe 17 Disemba 2019, ili muda wa miezi mitatu na siku 17 ulikuwa umepita. Mahakama iliamua kwamba kipindi cha miezi 3 na siku 17 ni cha kuridhisha kwa mujibu wa maana ya Kanuni ya 50(2)(f).

Mwisho, Mahakama ilipata kwamba kesi hiyo haikuwa imekamilishwa kabla ya mahakama nyingine ya kimataifa na hivyo ilikuwa inatii Kanuni ya 50(2)(g) ya Kanuni hizo. Kwa hivyo, Mahakama ilihitimisha kuwa Ombi hili lilikuwa na ukubalifu.

Kisha Mahakama ilifikiria kama Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka haki za Mwombaji za usawa mbele ya sheria, ulinzi sawa wa sheria, utu na kesi inayoendeshwa kwa haki, vinavyolindwa na Ibara za 3(1), (2), 5 na 7 za Mkataba, mtawalia. Hata hivyo, Mahakama ilibainishwa kwamba pingamizi kuu katika Ombi hilo ilijikita katika Ibara ya 7(1) ya Mkataba, haki ya Mwombaji ya kusikilizwa kwa kesi yake, hivyo basi, ukiukwaji huu wa nadai ulishughulikiwa kwanza.

Mwombaji alitoa malalamiko tofauti dhidi ya mahakama za ndani ambazo kutenda au kutotenda kwake alidai kuwa kulikiuka haki zake. Malalamiko haya yalihusu (i) ushahidi ambao ulisababisha kutolewa kwa hatia, (ii) uwezo wa mkalimani, na (iii) kunyimwa dhamana.

Katika dai linalohusiana na ushahidi ambao uliwezesha upatikanaji wa hatia kutolewa, Mahakama ilirejelea maamuzi yake ya awali, ambapo ilisema kwamba mahakama za ndani zinatabuliwa kwingi kwa kutathmini viwango vya uwezekano wa ushahidi fulani. Ikiwa mahakama ya kimataifa ya haki za binadamu, Mahakama haiwezi kuchukua jukumu hili kutoka kwa mahakama za ndani na ichunguze utondoti na upekee wa ushahidi unaotumiwa katika kesi za ndani. Hata hivyo, Mahakama inaweza, katika kutathmini jinsi kesi za ndani zinavyoendeshwa, kuingilia kati ili kutathmini iwapo kesi za ndani, ikiwa ni pamoja na tathmini za ushahidi, zilifanywa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Katika kesi hii ya sasa, baada ya uchunguzi wa kina wa rekodi, Mahakama ilibaini kwamba Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa zilichukua muda kuchunguza, kutathmini na kuthibitisha uaminifu wa Ushahidi pamoja na madai ya ua ukiukaji wa taratibu, na kupata

kwamba mashtaka dhidi ya Mwombaji yalithibitishwa bila shaka yoyote. Kwa hivyo, Mahakama iliona kuwa namna kesi zilizvyoendeshwa katika mahakama za ndani, pamoja na uzingatiaji wa ushahidi, haikudhihirisha makossa yoyote au upotovu wa haki uliohitaji uingiliaji kati wake. Kwa hiyo, Mahakama ilitupilia mbali madai ya Mwombaji na kushikilia kuwa Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki yake ya kusikilizwa, inayolindwa na Ibara ya 7(1) ya Mkataba.

Katika dai linalohusiana na uwezo wa mkalimani, Mahakama ilirejelea uamuzi wake wa awali katika kesi ya *Armand Guehi dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,* ambapo iliamua kwamba kila mshtakiwa ana haki ya kuwa na mkalimani ambacho ni kipengele cha kusikilizwa kwa kesi kwa haki chini ya Ibara ya 7(1)(c) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) na kwamba katika hali ambapo mshtakiwa hawezi kuelewa au kuzungumza lugha inayotumiwa mahakamani, ana haki ya kupata mkalimani. Katika kesi hii, Mahakama iliamua kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka Ibara ya 7(1)(c) ya Mkataba, ikisomwa pamoja na Ibara ya 14(3)(a) na (f) ya ICCPR, juu ya haki ya kujitetea kuhusu haki ya kusaidiwa na mkalimani, kama vile ukweli ulivyobaini kuwa uwezo wa Mwombaji wa kujitetea haukuathiriwa na suala hilo la lugha, ikichukuliwa, miongoni mwa mambo mengine, kwamba ukalimani ulitolewa kutoka kwa Kiswahili hadi Kichina na kinyume chake na kwamba aliwakilishwa na wakili wakati wa kesi hiyo na kesi ya rufaa.

Katika madai yanayohusu kunyimwa dhamana, Mahakama iliona kuwa Mkataba haumhakikishii mshatakiwa kwa uwazi haki ya kupewa dhamana katika kifungu chochote chake. Hata hivyo, ICCPR, katika Ibara ya 9(3), inathibitisha kuwa kuzuiliwa kwa watuwanaotuhumiwa kufanya uhalifu kunapaswa kuwa hatua ya kipekee. Wale wanaosubiri kesi zao kusikilizwa wanapaswa kupewa dhamana isipokuwa kama hali mahususi zinalazimu wawekwe kizuizini, kama vile haja ya kudumisha uadilifu wa kesi na kuzuia hatari ya kutoroka. Mahakama ilisisitiza kuwa uamuzi wa kumpa au kutompa mshtakiwa dhamana huhitaji tathmini ya kibinafsi, kwa kuzingatia ukweli wa kipekee wa kila kesi na mazingira mahususi ya Mwombaji. Mahakama pia ilibainisha kuwa kunaweza kuwepo na hali zinazosababisha kunyimwa kwa dhamana. Katika kesi ya sasa, Mahakama iliona kuwa Mahakama ya Hakimu, katika hukumu yake iliyotolewa tarehe 24 Novemba 2015, ilizingatia ipasavyo sababu mbalimbali za kumnyima dhamana Mwombaji na mshtakiwa mwenzake, ikiwa ni pamoja na uzito wa shtaka dhidi ya Mwombaji, uzito wa adhabu inayoweza kutolewa, ulazima wa kuhakikisha uwepo wa Mwombaji katika muda wote wa kesi, pamoja na hatari ya kutoroka na athari kubwa kwa kesi ikiwa hilo litatokea. Kwa kuzingatia yaliyotangulia, Mahakama iliamua

kwamba uamuzi wa mahakama ya ndani wa kumnyima dhamana Mwombaji hauoneshi makossa yoyote ya wazi yanayohitaji uingiliaji kati wake. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali dai la Mwombaji na kuamua kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki ya Mwombaji ya kusikilizwa, inayolindwa katika Ibara ya 7(1) ya Mkataba, ikisomwa pamoja na Ibara ya 9(3) ya ICCPR, kuhusu haki ya Mwombaji kupata dhamana.

Kuhusu dai la kukiukwa kwa haki ya utu kutokana na adhabu aliyopewa, mahakama iliona kuwa mahakama iliyosimamia kesi ilitoa adhabu hiyo kulingana na sheria, kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Kiuchumi na Uliopangwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyapori. Mahakama ilibainisha zaidi kuwa kufuatia rufaa yake mbele ya Mahakama Kuu, Mwombaji aliondolewa hatia katika shtaka la kwanza na kwamba ni upatikanaji na hatia, hukumu na maagizo yaliyotolewa dhidi yake katika mashtaka ya pili na tatu yaliyothibitishwa. Mahakama ilizingatia zaidi kuwa mahakama ya ndani ilitia maanani uzito wa kosa wakati wa kutoa hukumu, kama inavyoruhusiwa na sheria. Katika hali hizi, Mahakama ilibainisha kuwa Mwombaji alishindwa kuthibitisha ukiukaji uliodaiwa kutokea na ikaamua kuwa Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki yake ya utu na heshima, iliyohakikishwa katika Ibara ya 5 ya Mkataba, kuhusu hukumu aliyopewa.

Kuhusu dai la ukiukwaji wa haki ya usawa mbele ya sheria na haki ya ulinzi sawa wa sheria, Mahakama ilisema kwamba Mwombaji alikuwa ameshindwa kueleza msingi wa ukiukaji unaodaiwa wa Ibara ya 3 ya Mkataba. Pia Mahakama ilibainisha kuwa Mwombaji aliweza kutumia njia zote za kisheria zinazopatikana kwake na kwamba aliweza kujitetea kulingana na ulinzi unaotolewa na sheria. Kwa hivyo, mahakama iliamua kuwa Mwombaji hakuthibitisha dai la ukiukaji na ikaamua kuwa Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki zake za usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria inayolindwa chini ya Ibara ya 3 ya Mkataba.

Baada ya kuamua kuwa Taifa Lililoshtakiwa halikukiuka haki zozote za Mwombaji, Mahakama inatupilia mbali maombi ya fidia. Kuhusu gharama, Mahakama iliamua kwamba kila mdaawa atajilipia gharama zake.

**Taarifa zaidi**

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na matini kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, zinaweza kupatikana kwenye tovuti katika: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0662019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Ofisi ya Msajili kwa baruapepe registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha kuna ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka juu ya kesi na migogoro yote inayowasilishwa kwake kuhusu ufasiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na hati nyingine yoyote iliyoidhinishwa na Mataifa yanayohusika. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu katika www.african-court.org.*